NAMBA YA KITAMBULISHO CHA MWANAFUNZI ____________________

# Tunahitaji usaidizi wako!

## ...na tutakulipa kwa wakati wako.

**Successful Families 2020** ni juhudi ya pamoja kati ya mashirika yasiyokuwa ya biashara ya IRCO, Latino Network, Metropolitan Family Service, NAYA Family Center na SEI yanayo jitihadi kuimarisha matokeo ya elimu kwa wanafunzi wasiokuwa weupe kwa kuwapa tuzo na kuwafhamisha mila na tamaduni katika programu.

Successful Families 2020 inashirikiana na **H.B. Lee Middle School**, **Reynolds Middle School** na Reynolds High School ili kuhimiza mazingira imara ya shule na kuhakikisha kuwa wanafunzi wasiokuwa weupe wanafuzu shule ya upili wakiwa tayari kwa chuo kikuu na kazi.

United Way ya Columbia-Willamette na Portland State University wanashirikiana na haya mashirika yasiyokuwa ya biashara na hizi shule pia ili kufahamu zaidi jinsi programu zao zinasaidia wanafunzi ndani na nje ya shule. Kufahamu zaidi kuhusu waliyoapitia wanafunzi na wazazi/walezi wakiwa kwenye programu hizi, tunahitaji usaidizi wako na tutakulipa kwa wakati wako!

Tutakuwa tunafanya utafiti wakati wa mwaka wa shule 2017-18 kwa wanafunzi na wazazi/walezi wao katika programu H.B. Lee, RMS na RHS wanaofaidika na programu zinazoshirikiana na Successful Families 2020.

Huenda tutawasiliana na wanafunzi na wazazi ili washiriki katika udadisi, makundi ya mwelekeo au aina nyengine ya mahojiano ili kufahamu vyema zaidi kuhusu waliyopitia katika programu na shule hizi. Kushiriki ni kwa hiari. Ukipendelea kutusaidia, tafadhali tia sahihi fomu ya idhini iliyoko kwenye pakiti hii.

Huduma za tafsiri na ukalimu zinapatikana zinapohitajika.

**ASANTE KWA WAKATI WAKO!**

# Maelezo ya Idhini

**Nyaraka zifwatazo zinaeleza idhini zinazopeanwa na wazazi, walezi na wanafunzi. Kama unakubali, tia sahihi ukurasa wa mwisho wa Fomu ya Idhini.**

**Kama mwanafunzi na mzazi/mlezi pamoja wanatia sahihi fomu hii, una:**

- ☐ **Unaturuhusu kuwasiliana nawe wakati wa mwaka wa shule 2017-18 na ikiwezekana mwaka wa shule 2018-19 ili ushiriki kwenye udadisi**

- ☐ **Tujulisha kwamba unakubali kushiriki katika utafiti na kukamilisha maswali kuhusu yale waliyopitia wanafunzi na familia ndani na nje ya shule.**

- ☐ **Unaturuhusu kutazama na kutumia rekodi zako za mwanafunzi kama vile za kuhudhuria shule, matokeo ya mitihani, alama za mitihani, nidhamu na kufuzu**

- ☐ **Unaturuhusu kutumia rekodi za programu/huduma za Familia Zinazofaulu 2020 ambazo washiriki huenda wanazo kukuhusu (mwanafunzi na/au familia) ili kutuwezesha kuelewa vyema yale muliyoyapitia**

- ☐ **Fahamu kwamba hakuna majibu ya udadisi wa mtu yoyote binafsi (mwanafunzi au mzazi) yataonyeshwa wengine hadharani na hayataonyeshwa walimu, wafanyikazi wa shule, wazazi wengine na wafanyikazi wa mashirika yasiyokuwa ya biashara**

- ☐ **Fahamu kuwa kushiriki katika udadisi huu ni kwa hiari, na unaweza kuwacha wakati wowote**

# <u>Fomu ya Idhini</u>

*<u>Idhini Fahamu ya Jumla, ikiwa ni pamoja na kupatiwa rekodi za wanafunzi kwa utafiti huu:</u>*
***Mwongozo wa Mafanikio ya Elimu kwa Wanafunzi Wasiokuwa Weupe:***
***Kuamua Sera Bora na Taratibu Imara katika Shule za Umma***

Wazazi na wanafunzi wao wanakaribishwa kushiriki katika utafiti unaongozwa na Ann Curry-Stevens kutoka Shule ya Kazi za Jumuiya (School of Social Work) Portland State University. Utafiti hii unahusu wanafunzi na familia ambao wao ni sehemu ya programu za usaidizi wa elimu na tamaduni (kama zile zinazopeanwa na Immigrant and Refugee Community Organization, Latino Network, Metropolitan Family Service, Native American Youth and Family Center na Self-Enhancement, Inc.) Wazazi/walezi na mwanafunzi wao wamekaribishwa kushiriki kwa sababu mwanafunzi amesajiliwa katika moja ya programu hizi.

Kama mzazi ataamua kushiriki katika udadisi huu, huenda tutamuomba afanye udadisi au ashiriki kwenye makundi ya mwelekeo. Udadisi utauliza maswali kuhusu familia, mapato, mbari/kabila, na hali ya kuishi, pamoja na maswali kuhusu yale waliyoapitia wazazi na wanafunzi, shule na darasa. Kila udadisi utachukuwa dakika 30-45 kukamilisha. Mzazi/mlezi atapokea malipo kila mara anapofanya udadisi.

Kama wazazi wataamua kuruhusu vijana wao washiriki, huenda tutawaomba vijana wakamilishe udadisi au washiriki kwenye makundi ya mwelekeo katika mwaka wa masomo wa 2017-2018. Huenda tutafwatilia wanafunzi baada ya mwaka wa masomo 2017-2018 kwa udadisi wa mwisho. Utafiti huu utamuuliza mwanafunzi atoe maoni yake na hisia zake kuhusu shule, walimu, jumuiya, kujitambua kitamaduni na kimbari, na kuhusu elimu kwa jumla. Kila udadisi huenda utachukuwa dakika 30-45 kukamilisha, lakini wanafunzi watapokea fidia kila mara wanapomaliza udadisi.

Tunaomba ruhusa tutazame rekodi za masomo za mwanafunzi, ambazo huenda zitajumuisha kitambulisho cha mwanafunzi, darasa alilofikia, anavyohudhuria shule, matokeo ya mitihani, alama anazopata, hali ya kiuchumi, matokeo ya mitihani ya kupima uwezo wa masomo, nidhamu na kufuzu. Tunakusanya maelezo mengi kwasababu tumeombwa na mashirika tutambue ni mambo gani yanafaulu na gani hayafaulu kuwasaidia wanafunzi wafanye vyema katika masomo.

Tutatazama rekodi za wanafunzi kwa mwaka huu wa masomo (2017-2018), kwa miaka miwili ijayo ya masomo (2018-2019 na 2019-2020), na kwa mwaka wanaotazamiwa kufuzu shule ya upili. Ripoti za kuhudhuria na za nidhamu zitapeanwa na wafanyikazi na kijana ili wao nao waweze kusaidia vyema zaidi vijana. Rekodi nyengine za shule, na pia chochote ambacho mzazi au mwanafunzi anatwambia kwenye udadisi, kitawekwa kwa usiri. Ni watafiti ambao ni sehemu ya utafiti huu pekee watakaoweza majibu ya anaefanya udadisi. Hatutapatiana majibu yoyote yenye majina ya wahusika au maelezo binafsi ya mzazi au mwanafunzi na walimu, wafanyikazi wa shule, wazazi wengine, au wafanyikazi wa mashirika ya jumuiya yanayofanya kazi na mwanafunzi.

Uamuzi wako (wa mzazi na mwanafunzi) kushiriki katika utafiti huu ni wa hiari. Hata kama mzazi atapeana idhini ili kijana ashiriki, kijana bado anaweza kuamua hatashiriki. Wazazi sio lazima washiriki kama hawataki, na wanaweza kuwacha kushiriki wakati wowote bila hatua hiyo kuathiri uhusiano wa mzazi au kijana na shirika la jumuiya, shule, United Way, au Portland State University. Wazazi na wanafunzi sio lazima washiriki katika utafiti huu ili wawe katika programu zinazopeanwa na shirika lako la jumuiya.

Wazazi na wanafunzi hawatapata mafao yoyote spesheli kwa kushiriki katika udadisi, isipokuwa kwa kutusaidia kutambua zaidi ni mambo gani yanafaulu na gani hayafaulu kuboresha mafanikio ya wanafunzi. Kuna wasiwasi kwamba wazazi au wanafunzi huenda wakapatwa na hisia za kutokuwa huru au kutokuwa na faragha wanapoulizwa maswali fulani. Mzazi au mwanafunzi anaweza kuruka swali lolote au awache kushiriki wakati wowote bila kuadhibiwa. Tutachukuwa hatua zote tuwe waangalifu ili kuepuka namna yoyote ya kupoteza usiri kwa kuweka rekodi za karatasi ndani ya ofisi zinazofungwa na kuweka rekodi za umeme kwenye kompyuta imara zinazolindwa na neno siri (password) imara.

Yeyote kati yenu akiwa na swali aina yoyote kuhusu mradi huu wa utafiti au kushirki, wasiliana na Ann Curry-Stevens kwa 503-725-5315. Kama una wasiwasi kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti, tafadhali wasiliana na ofisi ya utafiti ya PSU Office of Research Integrity katika Market Center Building Suite 620, Portland State University, au piga simu I 503-725-2227.

RUHUSA YA MZAZI: **Kwa kutia sahini kiboksi cha manjano hapo chini, unasema kwamba unaelewa maelezo yalioandikwa hapo juu, kwamba unapeana idhini kijana wako ashiriki katika utafiti huu, na kuwa unakubali kushiriki katika utafiti huu. Unakubali pia kuidhinisha kutolewa na kubadilishwa kwa maelezo ya mwanafunzi wako ikiwa pamoja na jina, # ya kitambulisho, darasa lake, matokeo ya mitihani, alama za masomo, hali ya kiuchumi, kuhudhuria, na nidhamu katika ya Reynolds School District, Portland State University, United Way of Columbia-Willamette, na wafanyikazi wa utafiti na udadisi wanaofanya utafiti huu.**

***Namna ya Kuwasiliana na Mzazi*** barua pepe: @ ______________________ simu: ______________________

Jina la Mzazi/Mlezi (Andika) | Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe

Jina la Mwanafunzi (Andika)

RUHUSA YA MWANAFUNZI: **Kwa kutia sahini kiboksi cha manjano hapo chini, unasema kwamba unaelewa maelezo yalioandikwa hapo juu, na kuwa unakubali kushiriki katika utafiti huu.**

***Namna ya Kuwasiliana na Mwanafunzi*** barua pepe: @ ______________________ simu: ______________________

☐ *Tafadhali weka alama kama wewe, mwanafunzi, una zaidi ya miaka 18.*

Sahihi ya Mwanafunzi | Tarehe